# Chuo cha CBCTC Namtumbo kilivyofanikiwa kutoa mafunzo ya uhifadhi wa maliasili kwa Jamii

**Na Albano Midelo**



CHUO cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) kilichopo katika Kijiji cha Likuyu Sekamaganga wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma kimepata mafanikio makubwa katika suala zima la uhifadhi wa maliasili.

CBCTC ni Chuo pekee cha utoaji wa mafunzo ya uhifadhi wa maliasili kwa jamii barani Afrika na kwamba hapa nchini katika vyuo vya uhifadhi ,hakuna chuo kinachotoa mafunzo yanayofanana na chuo hiki,hali hiyo ndiyo inakifanya kuwa ni chuo cha kipekee nchini.

Mkuu wa CBCTC Jane Nyau akizungumza katika mahafali ya kozi ya Askari wanyamapori wa vijiji(VGS) yaliofanyika Juni 24,2018

,ameyataja miongoni mwa mafanikio ya chuo hicho kuwa ni kutoa mafunzo kwa wananchi 4512 kati yao  wanaume ni 3804 na wanawake 708.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo,Chuo hicho ambacho kilianzishwa mwaka 1995 kinatekeleza sera ya wanyamapori inayosisitiza ushirikishwaji wa jamii katika uhifadhi wa rasilimali za maliasili,lengo kuu likiwa ni kuijengea jamii uwezo kwa njia ya mafunzo ili kuiwezesha kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.

Hata hivyo ili kufikia malengo hayo,Nyau anataja aina mbili ambazo zinatolewa na CBCTC kuwa ni mafunzo ya Askari Wanyamapori wa vijiji(VGS) ambayo inatolewa kwa miezi mitatu na mafunzo ya viongozi wa serikali na Kamati za Maliasili za vijiji ambayo hutolewa kwa mwezi mmoja.

“Kozi namba 63/2018 ambayo mafunzo yake yanahitishwa leo ilianza Machi 25,2018 ikiwa na jumla ya washiriki 56 kati yao wanaume 38 na wanawake 18,washiriki 55,wanatunukiwa vyeti,mshiriki mmoja ameshindwa kuhitimu kutokana na matatizo ya kiafya”,anasema Nyau.

Anawataja washiriki hao kuwa wanatoka katika Wilaya na Jumuiya mbalimbali ikiwemo Namtumbo na Tunduru mkoani Ruvuma,Nanyumbu na Nachingwea mkoani Mtwara.Liwale,Rufiji na Mbulu.

Amesema mafunzo hayo yametolewa kwa njia ya nadharia na vitendo ambapo iliwalazimu wanachuo kwenda porini kwa ajili ya kutekeleza kwa vitendo waliojifunza kwa nadharia darasani.



Hata hivyo kwa ufadhili wa USAID kupitia mradi wake wa Promoting Tanzanian Envroment,Conservation and Tourism(PROTECT),chuo hicho kimefanikiwa kudurusu na kuandaa mitaala ya kozi zake za VGS na viongozi ili kuweza kujibu changamoto za uhifadhi ambazo hazikuwepo kwenye mtaala wa awali.

“Vitu vilivyoongezwa kwenye mtaala ulioboreshwa ni utatuzi na mbinu za kujikinga na wanyamapori wakali na waharibifu,matumizi ya GPS na ramani katika doria,ujasirimali ambao ni rafiki wa mazingira na masuala mtambuka.

Ameongeza kuwa katika mtaala ulioboreshwa muda wa mafunzo umeongezeka ambapo sasa kozi za mafunzo ya Askari wanyamapori vijijini zinatolewa kwa miezi mitatu badala ya wiki sita za awali na kozi za mafunzo viongozi wa Kamati za Maliasili za vijiji zinatolewa kwa mwezi mmoja badala ya wiki mbili.

“CBCTC imeandaa mtaala wa kozi ya waongoza watalii itakayotolewa kwa mwaka mmoja,mtaala huo umewasilishwa NACTE kwa ajili ya kuthibitishwa,na kozi hii inatarajiwa kuanza mwaka wa fedha wa 2018/2019,kozi hii itatolewa sanjari na kozi fupi za VGS”,anasisitiza Nyau.

Licha ya mafanikio ya chuo hicho,Nyau anazitaja changamoto zinazokikabili chuo hicho kuwa ni upungufu wa watumishi ambapo chuo hicho hivi sasa kina watumishi sita tu,uchakavu wa

majengo,ukosefu wa baadhi ya majengo muhimu kama maktaba,stoo,chumba cha kompyuta na darasa lililopo ni dogo halikidhi mahitaji chuo kinapopata wanafunzi wengi.

Akizungumza katika mahafali hayo Mwakilishi wa  Shirika la USAID PROTECT Thadeus Binamungu amesema shirika hilo limetoa msaada wa vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Zaidi ya shilingi milioni 46 ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazokikabili chuo cha CBCTC Likuyu.



Amesema Shirika la PROTECT ambalo linajishughulisha na kuendeleza mazingira,uhifadhi na utalii Tanzania,limetoa jenereta moja ambayo itasaidia kufua umeme ambao unatumika katika chuo hicho.

Misaada mingine ameitaja kuwa ni viona mbali kumi,kompyuta mpakato tano,powerpoint mbili,na vitabu 40 kwa ajili ya kozi ya waongoza watalii ambayo itatolewa kwa mwaka mmoja ambayo itakiwezesha chuo hicho kusajiliwa NACTE na kuzalisha watalaam wa kutosha ili kuendana na dhana ya kukuza utalii ukanda wa kusini.

Hata hivyo kwa mujibu wa Binamungu kati ya vitabu vilivyotolewa,vitabu 12 ni vya wanyama wanyonyeshao, vitabu 12

vya ndege,vitabu 10 vya mimea na vitabu sita vya wanyama jamii ya mijusi na kwamba vifaa hivyo vimetolewa rasmi kwa ajili ya kusaidia na kurahisisha ufundishaji wa kozi ya waongoza watalii mara itakapoanza.

Akizungumza baada ya kuwatunuku vyeti wahitimu 55 katika chuo hicho,Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii Meja Generali Gaudence Milanzi ambaye sasa ni mstaafu amesema suala la usimamizi wa rasilimali za maliasili linahitaji ujuzi na weledi.



Amesema kutokana na hali hiyo ndiyo maana Wizara ya Maliasili na Utalii ilianzisha vyuo vya utoaji mafunzo vinavyohusiana na mafunzo ya uhifadhi wa maliasili hususan wanyamapori ambavyo vipo chini ya Wizara.

Chuo cha CBCTC Likuyu  kama jina lake linavyojieleza kilipewa jukumu la kuwajengea uwezo wananchi kwa njia ya kuwapatia

mafunzo ya uhifadhi wa maliasili kwa jamii kwa kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika uhifadhi na matumizi endelevu.

Meja Generali Milanzi ametoa rai kwa wahitimu kuwa walinzi hodari na makini mara baada ya kupata mafunzo hayo,sanjari na kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi wengine vijijini ili washiriki kikamilifu katika ulinzi wa rasilimali za Taifa ili ziweze kuwanufaisha wote.

“Ninyi kama Askari wanyamapori vijijini,mtakuwa hamzitendei haki jamii zetu na Taifa kwa ujumla endapo mtatumia ujuzi mlioupata kwa maslahi yenu binafsi,natarajia kwa kujali kizazi cha sasa na kijacho ninyi hamtakiuka maadili ya kazi yenu”,anasisitiza Milanzi.

Hata hivyo amesema licha serikali kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ujangili hapa nchini,bado ujangili dhidi ya tembo na wanyama wengine kama simba kwa kuwaua kwa sumu unaendelea kufanyika.

Amelitaja lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa ujangili wa aina zote dhidi ya wanyamapori unatokomezwa kwa asilimia 100 na kwamba pasiwepo kabisa na mnyama ambaye ameuawa na majangili.

**Mwandishi wa makala haya anapatikana kwa baruapepe albano.midelo@gmail.com,simu 0784765917**